JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

# KATIKA KAMATI YA MAUDHUI YA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA, DAR ES SALAAM

## SHAURI LA UKIUKAJI WA AGIZO LA SERIKALI KUHUSU KUTOSOMA HABARI ZA MAGAZETINI KWA UNDANI

## SHAURI NA. 04-2018/2019

## CLOUDS TELEVISION

# UAMUZI

## UAMUZI WA KAMATI YA MAUDHUI KUHUSU TUHUMA ZA UKIUKAJI WA AGIZO LA SERIKALI LA KUTOSOMA HABARI ZA MAGAZETINI KWA UNDANI

### 1.0 Utangulizi

1.1 Kituo cha Utangazaji cha Clouds Television cha Dar es salaam kinatuhumiwa kukiuka Agizo la Serikali lililotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo , Mhe. Dkt. Harrison Mwakyembe (Mb), tarehe 03 Mei, 2017 kwa watangazaji wa vituo vya Redio na Televisheni kutosoma kwa undani maudhui yaliyopo katika magazeti badala yake wasome vichwa vya habari pekee. Kimsingi, agizo hilo la Serikali lililenga katika kulinda soko la biashara ya uchapishaji, usambazaji, na uuzaji wa magazeti nchini.

1.2 Aidha, tarehe 15 Juni, 2017, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania iliviandikia barua vituo vyote vya utangazaji (ikiwa ni pamoja na kituo cha Clouds Television) na kuvitaka kuacha mara moja kusoma kwa undani habari za magazetini na badala yake wasome tu vichwa vya habari kwa mujibu wa agizo hilo la serikali.

1.3 Tarehe 28 Disemba, 2018, Kituo cha Clouds Television kinatuhumiwa kukiuka agizo la Serikali kupitia kipindi chake cha **Clouds 360** kilichorushwa kati ya saa 12.00 asubuhi na saa 4.00 asubuhi. Katika kipindi hicho, mtangazaji alisoma kwa undani habari mbali mbali zilizoandikwa katika magazeti ya Nipashe, Uhuru na Mtanzania kinyume na agizo lililotolewa na Serikali.

1.4 Kitendo cha kusoma taarifa hizo za magazeti kwa undani ni kupuuza kwa makusudi agizo la Serikali lililotolewa na Mheshimiwa Waziri tarehe 03 Mei, 2017 jijini Mwanza wakati wa kilele cha maadhimisho ya 26 ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari duniani.

1.5 Mtangazaji wa kipindi cha Clouds 360 alikiuka Agizo hilo la Serikali kwa kusoma habari za magazetini kwa undani kama ifuatavyo:-

***NIPASHE: Mawaziri wa JPM waliotaabika 2018***

***"Mwaka 2018 ambao umebakiza siku tatu kumalizika haukuwa mzuri kwa Mawaziri Wanne walioongoza idadi ya Mawaziri waliotumbuliwa tangu serikali ya awamu ya Tano ilipoingia madarakani mwaka 2015 kufikia Tisa;aidha mawaziri wanne waliopata misukosuko ambayo ilisababisha baadhi yao kutajwa hadharani na Rais John Magufuli wameshindwa kutekeleza wajibu wao ipasavyo kwa kadri iwezekanavyo...yali aaa aliyo.. maelekezo aliyoyatoa, mawaziri hao waliotumbuliwa kwa nyakati tofauti na Rais Magufuli walieleza sababu ya kutumbuliwa kwao....Habari inaendelea Ukurasa wa Nane"***

***NIPASHE: Gari la Mkuu wa Wilaya lazua mjadala mtandaoni***

***"Gari la Mkuu wa Wilaya ya Arumeru Mheshimiwa Jerry Muro limedaiwa kutumika vibaya kwa kubeba watu binafsi kwenda kwenye Mapumziko ya sikukuu ya Krismasi sehemu mbalimbali mkoani Arusha gari hilo lenye namba za usajili STL 3764 limedaiwa kumbeba rafiki yake kwenda kuzunguka mkoani humo kwa ajili ya mapumziko...picha ya gari hilo lenye bendera ya Taifa ilisambaa jana kwenye mitandao ya kijamii; rafiki huyo wa mkuu wa Wilaya William John Malecela maarufu kama Lemutuz huku akimshukuru kwa kumpa usafiri huo na kuzunguka nao tangu alipofika mkoani Arusha....eeeh! kwa hiyo hii ni habari ambayo imesambaa sana kwenye mitandao ya kijamii..."***

***UHURU Uk 2 : Njia Tano za wizi wa mabucha ya nyama ipo mpya ya kuwasha feni hiyo ukichomoka ushukuru...Kina baba ndio hupigwa Zaidi***

***" Katika uchunguzi wake Gazeti la Uhuru lilibaini kuwepo kwa njia mpya ya feni ambayo ni wateja wachache huijua na namna inavyotumika huwa ni kiujanja Zaidi,Mmoja wa wauzaji aliiambia Uhuru kuwa, kinachofanyika ni kuutegesha mzani katika namna ambayo feni iliyochezewa panga zake zinapowashwa hupunguza upepo kwa kiwango cha wastani kinachoamuliwa na mhusika ili mwishowe shinikizo la upepo liathiri kiasi cha nyama iliyopimwa...duh! Ahaa! Watu wabaya! Jamani mnaoenda ukiona umewashiwa feni ujue umeisha..."***

***MTANZANIA Uk 5: Mrema aiangukia serikali iruhusu mikutano ya siasa.***

***"Mwanasiasa Mkongwe nchini ambae pia ni mwenyekiti wa chama cha Tanzania Labor Party TLP Agustino Lyatonga Mrema ameipigia magoti serikali iruhusu mikutano ya kisiasa ifanyike ili kuviruhusu vyama vidogo ambavyo havina uwakilishi Bungeni...aah! Ili kuvinusuru...kumradhi! Vyama vidogo ambavyo havina uwakilishi Bungeni,akizungumza juzi jijini hapa Mrema aliiomba serikali ipitie upya uamuzi wake wa kuzuia mikutano ya hadhara kwani vyama vidogo vya siasa vinajenga nchi moja; Mrema ambae pia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Parole alisema hatua ya kuzuia mikutano bado inaendelea kudhoofisha vyama vidogo kwani kwa sasa hawana eneo la kusemea kama ilivyo kwa vyama vyenye wabunge; kwa mfano...gazeti Mtanzania limemnukuu Mrema..."Nataka serikali iruhusu mikutano ya kisiasa kwa vyama vyote vya siasa kwani vyama vyote vinajenga nchi" alisema Mrema.***

## 2.0 Wito wa kufika mbele ya Kamati ya Maudhui

Tarehe 02 Januari, 2019, Uongozi wa Kituo cha Clouds Television uliitwa mbele ya Kamati ya Maudhui kwa ajili ya kutoa utetezi wao kwa nini kituo hicho kisichukuliwe hatua kutokana na tuhuma za kukiuka Agizo la Serikali linalowataka watangazaji wa vituo vya Redio na Televisheni kutosoma undani wa maudhui yaliyopo katika magazeti na badala yake wasome vichwa vya habari pekee.

## 3.0 Kuangalia Kipindi cha Clouds 360 cha tarehe 28 Disemba, 2018

Kamati ya Maudhui na Uongozi wa Clouds Television waliangalia kipindi cha Clouds 360 cha tarehe 28 Disemba, 2018 kilichorushwa na Clouds Television ili kujiridhisha iwapo kituo hicho kilikiuka agizo tajwa la serikali au la.

## 4.0 Maelezo ya Utetezi ya Clouds Television.

Uongozi wa Clouds Television ulikubali kuwa kipindi kilichoangaliwa kilikuwa chao na kisha ulitoa maelezo yake ya utetezi kama ifuatavyo:-

4.1 **Dotto Bahemu** ambaye ni Msimamizi Mkuu wa Maudhui wa Clouds Televisheni alianza kwa kuipongeza Kamati kwa kazi inayoifanya na kisha kukiri kosa lililofanywa na mtangazaji wa Clouds 360 la kusoma habari za magazetini kwa undani kinyume na agizo la Serikali. Alieleza kuwa kosa lililofanyika ni la kibinadamu na lilisababishwa na kuwepo kwa mtangazaji mmoja katika kipindi baada ya wengine wawili kupata dharura. Aliendelea kueleza kuwa, wakiwepo watangazaji watatu huwa wanasoma vichwa vya habari tu na kujadiliana ili watazamaji waweze kuelewa lakini siku ya tukio alikuwepo mtangazaji mmoja tu na hivyo kulazimika kusoma magazeti kwa undani kidogo ili kuwaridhisha watazamaji. Alimalizia kwa kuomba

radhi na kusema kuwa ni mara ya kwanza kwa kosa hilo kufanywa na kituo chao tangu walipopokea agizo la Serikali.

4.2 **Hassani Ngoma** ambaye ni mtangazaji wa kipindi cha Clouds 360 alianza kwa kuiomba radhi Kamati kwa kosa alilolifanya na kuahidi kutolirudia tena. Alisema kuwa siku ya tukio alikuwa peke yake kwenye kipindi na aliletewa magazeti akiwa tayari hewani. Alliendelea kusema kuwa wakiwa watatu kwenye kipindi, mmojawapo (Sam Sasali) huwa anakuwa ameshasoma magazeti na hivyo huwa wanajadiliana kwa kupiga stori. Alimalizia kwa kusema kuwa huwa wanatekeleza agizo la Serikali lakini siku ya tukio walipatwa na dharura.

4.3 **Sam Sasali** ambaye pia ni Mtangazaji wa kipindi cha Clouds 360 alisema kuwa kama angekuwepo siku ya tukio, kosa hilo lisingefanyika na kwamba tangu agizo litolewe na Serikali, hawajawahi kulivunja. Aliomba radhi pia na kudai kuwa kosa hilo linasameheka.

4.4 **Nurdini Kabwanga** ambaye ni Mtayarishaji na Msimamizi wa Kipindi cha Clouds 360 alisema kuwa huwa anakuwa na mawasiliano na watangazaji wakati kipindi kinarushwa hewani, lakini wakati kosa linafanyika alishindwa kumzuia mtangazaji kwani wakati huo alikuwa akimtafuta Mheshimiwa Jerry Muro (Mkuu wa Wilaya ya Arumeru) kwenye simu. Alisema kuwa baadaye aliweza kumpa mtangazaji ishara na ndipo mtangazaji alipoacha kusoma magazeti yaliyofuata kwa undani. Pia, alisema kwamba hawakuweza kutafuta mtangazaji mbadala mapema kwa sababu dharura ya Sam Sasali ilitokea asubuhi wakati akitakiwa kuingia kwenye kipindi.

## 5.0 Majumuisho ya Utetezi

Katika kujumuisha utetezi wao, **Dotto Bahemu** alisema kuwa wamejitahidi sana kusema ukweli wa kilichotokea japokuwa utetezi wao hauondoi kosa. **Hassani Ngoma** alisema kuwa hawailaumu Kamati kwani inatekeleza agizo la Serikali, **Sam Sasali** aliendelea kuiomba radhi Kamati. **Nurdini Kabwanga** aliiomba Kamati iwaonee huruma itakapotoa uamuzi wake.

## 6.0 Tathmini ya Kamati

6.1 Kamati ya Maudhui imebaini kwamba, Kituo cha Clouds Television kupitia Kipindi chake cha Clouds 360 kimekiuka Agizo la Serikali la kutosoma habari za magazetini kwa undani kwa makusudi na kwa uzembe mkubwa na pia utetezi wake haukuwa wa msingi.

6.2 Kamati ya Maudhui imebaini kuwa kutokuwepo kwa watangazaji watatu katika kipindi hakuiondolei Kituo cha Clouds Television kosa, bali Kituo kimeonesha udhaifu mkubwa katika usimamizi, ubunifu na uendeshaji wa vipindi vyao.

## 7.0 Uamuzi wa Kamati

Baada ya kusikiliza na kutafakari kwa kina maelezo ya utetezi yaliyotolewa na Uongozi wa Clouds Televisheni, Kamati ya Maudhui imeridhika kuwa Kituo cha Clouds Televisheni kupitia kipindi chake cha Clouds 360 kimekiuka kwa makusudi na kwa uzembe mkubwa Agizo la Serikali la kutosoma habari za magazetini kwa undani kama ilivyoelezwa katika tathmini hapo juu.

Hivyo, Kamati ya Maudhui inaamua yafuatayo:-

7.1 Kituo cha Clouds Television kinapewa **Onyo Kali** na kukiagiza kutorudia kosa kama hili;

7.2 Kituo cha Clouds Television kinaamriwa kuomba radhi/msamaha Serikali na yeyote ambaye kwa namna moja au nyingine ameathirika na matangazo hayo kwa siku tano mfululizo kuanzia tarehe 7 – 11 Januari, 2019) katika kipindi chake kilekile cha Clouds 360 kwenye kipengele cha "Kunani Tanzania";

7.3 Kituo cha Clouds Television kinaamuriwa kuandika barua ya kuomba radhi/msamaha kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa kosa walilolifanya.

Uamuzi huu umetolewa na kusomwa Dar es Salaam siku hii ya tarehe **4** mwezi **Januari**, mwaka **2019**.

Haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu kwenye Baraza la Ushindani wa Haki Kibiashara (Fair Competition Tribunal – FCT) iko wazi ndani ya siku 21 (ishirini na moja) kuanzia leo.

**Uamuzi huu Umesainiwa na:**
**Bwana Joseph Method Mapunda**

**......................................**

**Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui**

TANZANIA COMMUNICATIONS REGULATORY AUTHORITY
P.O. Box 474
DAR-ES-SALAAM

**WAJUMBE WA KAMATI YA MAUDHUI:**

1. **Bwana Abdul Ramadhani Ngarawa......................................**
2. **Bwana Derek Kaitira Murusuri......................................**
3. **Bwana Jacob Gregory Tesha......................................**